BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Saba – Tarehe 23 Februari, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali PAC ya Mwaka 2019/2020 na 2020/2021.

## III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

138. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kuanzisha mfuko maalumu wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi. Katika jimbo la Dimani wapo vijana ambao wana uwezo wa kujiajiri na wana sifa za kupata mikopo hiyo ya uwezeshaji.

Je, ni vijana wangapi wa jimbo la Dimani ambao wamepata mikopo na ambao tayari wameanza kujiajiri wenyewe na wanachotaka ni msukumo tu wa Serikali.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

81. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Wapo askari wa vikosi vyetu vya SMZ walioumia wakati wakienda na kurudi kazini na walioumia wakiwa kazini wakitekeleza majukumu yao ya kazi, lakini wanajigharamia wenyewe kwa matibabu yao badala ya kutibiwa kwa gharama za Wizara kupitia Taasisi zake husika.

(a) Je, Wizara ina utaratibu gani juu ya hili.

(b) Vikosi vya SMZ vilikuwa tayari kujiunga na Bima ya Afya lakini Wizara ikawazuia. Je, kulikuwa na sababu zipi zilizopelekea kuwazuia huko.

(c) Ni lini askari wa vikosi vya SMZ wataunganishwa na Mfuko wa Bima ya Afya.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

43. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali inastahili pongezi kwa kuanzisha na kuendeleza Mfuko wa Barabara wa Zanzibar (Zanzibar Road Fund). Hata hivyo, inasikitisha kwamba fedha ya Mfuko huo hazitumiki ipasavyo kwa mujibu wa malengo yaliyowekwa.

(a) Je, kwa miaka mitano iliyopita (2017-2022), ni kiasi gani kilikusanywa kila mwaka kwa ajili ya Mfuko huo.

(b) Je, ni asilimia ngapi ya kiasi kilichokusanywa kilitumika kwa shughuli za Mfuko.

(c) Je, ni kwa nini, kwa kiasi kikubwa, fedha za Mfuko wa Barabara hazitumiki ipasavyo kwa mujibu wa malengo yaliyowekewa mfuko huo.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

76. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Uanzishwaji wa Serikali Mtandao (e-Government) ulikusudia, pamoja na mambo mengine, kurahisisha upatikanaji wa huduma, kuziba mianya ya rushwa isiyokuwa na sababu na kuongeza uwajibikaji, ili kujenga Serikali wezeshi (Accountable and Responsive Government). Hata hivyo, kwa nchi ndogo kama Zanzibar, Serikali Mtandao imechukua muda mrefu na gharama kubwa ikilinganishwa na ufanisi uliofikiwa:

(a) Je, Serikali Mtandao (e-Government) Zanzibar, iko katika hatua gani na lini itakamilika kusimamishwa nchi mzima.

(b) Je, hadi sasa, mradi wa kuanzisha Serikali Mtandao Zanzibar umeshagharimu kiasi gani.

(c) Je, ni yepi matarajio pindi Serikali Mtandao Zanzibar ikikamilika.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

25. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Wasanii katika tasnia zetu mbali mbali za sanaa wana athari katika kukuza au kudumaza mila, silka na tamaduni zetu.

(a) Je, Wizara inawafuatilia kwa karibu wasanii wanaodumaza mila, silka na tamaduni zetu.

(b) Je, ni hatua gani za kinidhamu Wizara imezichukua na itaendelea kuzichukua kwa wasanii wanaokiuka maadili yetu na kuvipotosha vizazi vyetu.

**Wizara ya Afya:**

41. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na jitihada nyingi zinazochukuliwa na Serikali yetu za kuboresha huduma za afya, bado zipo changamoto nyingi katika upatikanaji wa huduma bora ya afya hapa nchini mwetu.

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha Mfuko Maalum wa Afya

(Health Basket Fund), ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya hapa nchini.

(b) Je, ni wafadhili wepi ambao wana moyo wa kusaidia masuala ya afya sambamba na wafanyabiashara waliopo nje na ndani ya Zanzibar.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

109. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kushirikiana na benki ya CRDB imetoa boti za uvuvi na zile za wakulima wa mwani kwa njia ya mkopo, kwa lengo la kuwajengea uwezo zaidi wavuvi wetu pamoja na wakulima wetu wa mwani.

(a) Je, hadi sasa ni boti ngapi za uvuvi na za mwani zimetolewa.

(b) Je, ni kiasi gani cha pesa hadi hivi sasa kimerejeshwa kutoka kwa wavuvi hao pamoja na wakulima wetu wa mwani kutokana na mikopo ya boti hizi walizokopeshwa.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

29. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Serikali yetu inachukua juhudi tofauti za kuyafanyia matengenezo majengo ya Mji Mkongwe ili kuhakikisha majengo yaliyopo yanaendelea kubakia katika hadhi na uhalisia wake.

Je, kwa kiasi gani wataalamu wa Akiolojia wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale wanashirikishwa katika kufanya ‘Heritage Assessment Survey’ kabla na wakati wa harakati za uchimbaji na ujenzi unaofanyika katika manispaa yote ya Mji Mkongwe Zanzibar.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

10. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa baadhi ya kampuni za usafiri na usafirishaji baharini huamua kujenga gati (jet) kwa ajili ya kuteremshia na kuweka abiria wao kabla ya kuingia kwenye vyombo na baada ya kuteremka katika vyombo hivyo, kama vile wanavyofanya AZAM MARINE Co. LTD pale Dar es Salaam na bandari ya Malindi Unguja.

Je, ni lini Serikali itaendelea kuwashawishi wawekezaji katika sekta ya usafiri wa bahari, kujenga maeneo ya kuteremshia na kukaa abiria Pemba kama vile ilivyo Unguja na Dar es Salaam.

14. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Usafi unahitajika sana katika viwanja vya ndege, ambapo miongoni mwa vitendea kazi vinavyotumika katika usafi huo ni pamoja na matrekta. Hata hivyo, katika Uwanja wa Ndege wa Pemba, trekta linalotumika kwa usafi hivi sasa ni bovu na kila siku linafanyiwa matengenezo bila ya uwepo wa mafanikio.

Je, ni lini Serikali itanunua trekta jipya la kisasa ili kuweza kurahisisha utendaji wa kazi za usafi uwanjani hapo.

131. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza sana Serikali hususan Rais wetu Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuboresha na kuzitengeneza njia za ndani kwa kiwango cha barabara zinazotumika kama barabara kuu. Nikiri kwanza jimbo la Mwanakwerekwe ni miongoni mwa wanufaika wa ujenzi wa njia hizo.

Je, ni lini Wizara itaifanyia marekebisho njia kubwa ya Meli Nne Makaburini hadi Kidatu, huku ikizingatiwa kwamba njia hii ni kiungo kikubwa sana cha watu na mali zao wanaotembea kwa miguu na vipando vyao.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

98. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Nawapongeza wakulima wetu wa Zanzibar kwa kuendeleza kilimo cha aina ya mazao na matunda mbali mbali ambayo hapo awali hayakuaminika kama yanaweza kuota na kuvunwa katika nchi yetu, ikiwa pamoja na njugumawe na maharage. Hata hivyo, wananchi wengi wa Unguja na Pemba bado hawajapata utaalamu wa kulima njungumawe na maharage.

Je, Wizara imejipanga vipi kuwapatia wataalamu na kuwahamasisha wakulima kulima kilimo hiki Unguja na Pemba.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

99. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika majibu yako ya msingi ya Mkutano wa Baraza uliopita, Mhe. Waziri uliahidi kuwapelekea umeme wananchi wa kijiji cha Kivumoni kilichopo shehia ya Mtambwe Kusini, katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka (mwezi wa Disemba 2022), lakini kwa bahati mbaya hadi hii leo huduma hiyo haijapelekwa.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi hao.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali PAC ya Mwaka 2019/2020 na 2020/2021.

Zanzibar,
23 Februari, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.